

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Mkopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025.

Mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya wadau (Public Hearing) utafanyika siku ya **Jumatano tarehe 29 Aprili, 2026 kuanzia saa 4:00 asubuhi** katika Ukumbi wa Msekwa, Bungeni Jijini Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huo, Kamati inawaalika wadau wote kufika kwenye Mkutano huo na kuwasilisha maoni yao kabla haujapelekwa katika hatua nyingine.

Aidha, maoni yanaweza pia kuwasilishwa kwa njia ya posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia Barua pepe ya cna@bunge.go.tz

Muswada huo unaweza kupakuliwa katika tovuti ya Bunge, <https://www.parliament.go.tz/bills-list>

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

17 Aprili, 2026.

1/1



[bungetz1](#) | [bunge_tz](#) | [bunge.tanzania](#) | Bunge TV | www.parliament.go.tz